

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA WAZIRI MKUU

Anwani ya Simu: "WAZIRI MKUU"  
Simu Nambari: +255 22112847  
Nukushi: +2255 2116798  
Barua pepe: [ps@pmo.go.tz](mailto:ps@pmo.go.tz)  
Unapojibu Tafadhali taja:



2 Mtaa wa Magogoni,  
S. L. P. 3021,  
11410 – DAR ES SALAAM

Kumb. Na. **PM/P/2/567/94**

**27 Desemba, 2016**

✓ Bw. Abraham S. Sangiwa,  
Mwenyekiti wa Mpito,  
Kamati Maalum ya Watanzania Waishio Nje,  
**TORONTO, CANADA.**

**YAH: UTAMBULISHO RASMI WA KAMATI  
MAALUM YA WATANZANIA WAISHIO NJE**

Tafadhali rejea kichwa cha habari hapo juu na barua yako ya tarehe 21 Novemba, 2016 kuitambulisha Kamati yako kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na kuomba miadi ya kukutana na kufanya naye mazungumzo ya ana kwa ana.

Baada ya kusoma barua hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshukuru kwa barua na pongezi kwa Serikali.

Kuhusu ombi la kukutana na kufanya naye mazungumzo, kimsingi yuko tayari kukutana nanyi muda wowote baada ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuwa imeratibu miadi hiyo. Hivyo, mnashauriwa kuwasiliana na Wizara hiyo, ili kupata utaratibu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu amewasihi diaspora wawe kitu kimoja na wafanye kazi kwa bidii. Aidha, amesisitiza kwamba jitihada za kuwaunganisha Diaspora zifanyike kwa umakini na maridhiano ili zisivunje au kudhoofisha Jumuiya za Diaspora zilizopo.

Ninakushukuru kwa ushirikiano wako.

A handwritten signature in black ink, appearing to read 'Mtibora'.

Abdallah M. Mtibora

Kny: **KATIBU WA WAZIRI MKUU**

**Nakala:**

Katibu Mkuu,  
Wizara ya Mambo ya Nje na  
Ushirikiano wa Afrika Mashariki,  
20 Barabara ya Kivukoni,  
S.L.P. 9000,  
**11466 DAR-ES-SALAAM.**